# HOTUBA YA MHE. ANNA E. MGHWIRA, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA KUKABIDHI MWENGE WA UHURU MKOA WA TANGA TAREHE 22/09/2017

- Mheshimiwa Martine Shigela, Mkuu wa Mkoa wa Tanga;
- Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa – Bw. Amour Hamad Amour;
- Ndugu Wakimbiza Mwenge Kitaifa Mwaka 2017;
- Ndugu Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga;
- Ndugu Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa wa Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga;
- Viongozi wa Madhehebu ya Dini;
- Viongozi wa Taasisi mbalimbali;
- Waandishi wa Habari;
- Wananchi wote tuliopo hapa;
- Mabibi na Mabwana:

Kwa niaba ya wananchi na viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro, ninamshukuru Mungu kutuwezesha kukamilisha Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka wa 2017 kwa **kishindo** na **salama.**

Ninawapongeza sana Wakimbiza Mwenge Kitaifa chini ya Uongozi madhubuti wa **Ndugu Amour Hamad Amour** kwa kazi nzuri ya kuukimbiza Mwenge wakati wote ulipokuwa Mkoani kwetu.

Aidha, natoa shukrani za dhati kwa Viongozi wa Serikali ngazi zote katika Mkoa wa Kilimanjaro na wananchi wote kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kufanikisha mbio hizi katika maeneo mbalimbali ambayo Mwenge ulipita.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;**

Kama tunavyofahamu Mwenge huu tuliupokea tarehe **15/09/2017** kutoka Uongozi wa Mkoa wa Manyara ukiwa salama pamoja na Wakimbiza Mwenge Kitaifa wakiwa na afya nzuri. Baada ya kuupokea Mwenge tumeukimbiza katika Halmashauri **saba** na leo tarehe **22/09/2017** tunaukabidhi kwa uongozi wa Mkoa wa Tanga ukiwa Salama unang'ara na Wakimbiza Mwenge Kitaifa wakiwa na afya njema na nzuri ya kuwawezesha kuendelea na Mbio za Mwenge.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;**

Katika kipindi chote Mwenge ulipokuwa Mkoani kwetu jumla ya miradi **42** yenye thamani ya shilingi **12,387,533,173/=** (shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia tatu na themanini na saba, laki tano na thelathini na tatu elfu na mia moja na sabini na tatu tu) ilizinduliwa, kufunguliwa, kuwekewa mawe ya msingi na kutembelewa. Utekelezaji wa miradi hii umechangiwa na wadau mbalimbali wa maendeleo na ninachukua nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;**

Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wanakupongeza wewe na Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa uelewa wenu wa ujumbe wa Mwenge mwaka huu unaosema **"Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo yetu".**

## 1. Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo yetu:

Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wamepokea kwa moyo mkunjufu ujumbe uliokuwa ukiutoa juu ya Viwanda.

Nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi na viongozi wenzangu wa Mkoa wa Kilimanjaro kukuahidi kuwa tutaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali kuwezesha Uchumi wa Viwanda kwa Maendleo ya Mkoa na nchi yetu.

**2. Malaria:**

Katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria, elimu kuhusu mbinu za kupambana na mbu aenezaye malaria imetolewa kwa ufasaha na wananchi wanashukuru sana kupata elimu hiyo pamoja na kuzijua athari zitokanazo na ugonjwa huu ambapo watoto na akina Mama wajawazito huathiriwa zaidi na ugonjwa huu. Katika kupambana na mbu anaye eneza ugonjwa huu, Halmashauri zimeagiza viuwatilifu ambavyo vitawekwa katika mazalia yote ya mbu kwa lengo la kuuwa viluwiluwi wanaozalisha mbu. Mpango wa Mkoa ni kuendelea kupunguza maambukizi ya malaria hadi kufikia chini ya asilimia **0.5** ifikapo mwaka **2020**.

**3. Mapambano dhidi ya UKIMWI:**

Wananchi wamepokea kutoka kwako ujumbe unaohamasisha mapambano dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI. Aidha, mmeshuhudia mikakati mbalimbali ya uhamasishaji juu ya upimaji virusi vya UKIMWI na kujikinga na UKIMWI kwa kupitia michezo, ngonjera, na mkaona huduma za afya za kuwahudumia waathirika wa Virusi vya UKIMWI.

Mkoa unaendelea na mapambano haya kwa lengo la kupunguza kiwango cha maambukizi kutoka asilimia **3.4** ya mwaka **2012** hadi asilimia **1.9** ifikapo mwaka **2020**.

**4. Madawa ya Kulevya:**

Elimu kuhusu kupiga vita uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya uliitoa kwa ufasaha na wananchi wanashukuru sana kupata elimu hiyo. Athari zitokanazo na dawa za kulevya ni kubwa ambapo watoto wadogo na wa mitaani wanapotumika kuziuza na wao huanza kuzitumia, hivyo kuathiri malezi na maadili yao katika jamii na hatimaye wanashindwa kushiriki katika masomo.

Aidha vita dhidi ya biashara na utumiaji wa mirungi katika maeneo ya Mkoa hususan Wilaya ya Same imedhihirisha kuwa madawa haya yameleta madhara mengi kiafya, kielimu na kijamii. Watoto wengi hushindwa kuhudhuria masomo, kudhoofika kiafya, uzururaji uliokithiri na uvunjifu wa amani hasa kwa vijana kutokana na ukweli kwamba madawa haya huathiri uwezo wa mwanadamu kufikiri.

Madhara haya ni makubwa katika jamii na Ujumbe wa Mwenge ulitoa umuhimu kwa wananchi kujikinga na tabia hii.

Katika uhamasishaji umejionea mbinu mbalimbali zinazotumika ikiwa ni pamoja na michezo ya kuigiza, ngojera na vilabu vya kuzungumzia suala hili. Katika kulipa kipaumbele suala hili Wilaya zetu sita (6) za Mkoa wa Kilimanjaro zimeanzisha vilabu vya kuzungumza athari na madhara ya utumiaji wa madawa ya kulevya.

**5. Rushwa:**

Mkoa wa Kilimanjaro upo katika mapambano dhidi ya Rushwa. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro nakuahidi kuwa elimu uliyoitoa dhidi ya rushwa itazingatiwa na hatimaye tutaweza kwa nguvu moja kuondokana na rushwa.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;**

Napenda kwa mara nyingine kukupongeza na kukushukuru wewe kwa kuongoza mbio hizi za Mwenge na kwa wakimbiza Mwenge Kitaifa kwa kazi kubwa mliyoifanya katika Mkoa wetu.

Ninawatakia afya njema katika kukamilishaji mbio hizi hadi mtakapofikia kilele tarehe **14/10/2017** huko Mkoani Mjini Magharibi.

**Mheshimiwa Mkuu  wa Mkoa wa Tanga;**

Naomba sasa nikukabidhi Wakimbiza Mwenge Kitaifa ambao kama unavyowaona wana **afya** njema na **ari kubwa** ya kuendelea na mbio za Mwenge wa Uhuru katika Mkoa wako wa Tanga.

1. **Bw. FREDERICK JOSEPH NDAHANI** - kutoka Mkoa wa Singida.

2. **Bi. VATIMA YUNUS HASSAN** -  kutoka Mkoa wa Kusini Pemba.

3. **Bw. BAHATI MWANIGUTA LUGODISHA** - kutoka Mkoa wa Geita.

4. **Bi. SALOME OBADIA MWAKITALIMA** - kutoka Mkoa wa Katavi.

5. **Bw. SHUKRAN ISIAM MSURI**  -  kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi.

6. **Bw. AMOUR HAMAD AMOUR** - kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa.

Baada ya kukukabidhi Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa; sasa niko tayari kukukabidhi Mwenge wa Uhuru ukiwa **salama** na **unameremeta.**

Mwisho kabisa; kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro tunawatakia afya njema na kila la kheri katika kuukimbiza Mwenge wa Uhuru Mkoani kwako kwa mwaka 2017.

**MWENGE HOYEE!!**

**KILIMANJARO HOYEE!!**